

HAKI YA NCHI NA KUSHIRIKI KATIKA KUIJENGA.

Imefasiriwa na profesa.Ayman Alasar

Hotuba ya Kwanza.

Shukrani ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu: {**Ingieni Misri kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu mukiwa na amani**}. Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake na ninashuhudia kuwa Muhammad S.A.W ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka sala salama na baraka kwake Mtume pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba wote na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

Baada ya utangulizi.

Kwa hakika haki ya nchi kwa wananchi wake ni katika haki za lazima zaidi na kusesitizwa, na kushiriki katika kujenga ni katika jukumu kubwa zaidi, kwani nchi ni moja ya mambo makuu sita ambayo yamezungumziwa na Sharia ya kati na kati kwa msisitizo mkubwa wa kulindwa, mtu huru hujitoa fidia nafsi yake kwa nchi yake.

Hakuna shaka kwa mwenye kufahamu dini yake kwa usahihi zaidi basi anafahamu kuwa uhusiano kati ya dini na dola sio uhusiano wa uadui na haitokuwa, na kuelewa vizuri dini kunachangia sana na kwa nguvu kubwa kujenga na kuleta utulivu wa nchi ya kisasa inayosimama kwa misingi ya imara ya utaifa, kama vile dola iliyobora haiwezekani kugongana na maumbile ya kibinadamu ambayo yanazungumzia imani sahihi.

Kwani Mtume wetu Muhammad S.A.W ameelezea maana ya kupenda nchi katika kauli yake *“Ni mji mzuri ulioje na ninaoupenda sana, lau watu wangu wasingenitoa kwako basi nisingeishi mji mwngine wowote zaidi yako”*.

Jambo la kupenda nchi sio kwa maneno tu au alama zinazoinuliwa bali ni pamoja na tabia na kujitoa muhanga, na katika haki za juu zaidi zinazotekelezwa kwa nchi ni pamoja na kujitoa muhanga kwa ajili ya nchi na kuilinda kutokana na hatari zozote zinazoweza tishia usalama wa nchi na watu wake, kwani kulinda nchi ni

katika misingi ya makusudio ya dini, na hii ndio njia ya watu wanaoheshimika na wakubwa wanaojitua kwa nchi yao, kwani utaifa na uzalendo wa kweli ni kujitua fidia pamoja na kujitua muhanga na kujifaharisha na nchi pamoja na ardhi yake pia kuheshimu bendera yake na wimbo wake wa taifa pamoja na asasi zake.

Utaifa na uzalendo wa kweli unapelekea kulinda mali za uma, kwani zenyewe ni msingi muhimu wa kuendeshea mambo ya nchi ikiwa ni pamoja na kutoa huduma na kuboresha maisha ya watu na jamii kwa ujumla, na kutoa mchango kupitia mali hizo za uma katika kujenga ustarabu wake, kwani anasema Mtume S.A.W *“Watu wanaharibu mali za Mwenyezi Mungu pasi ya haki basi siku ya Kiyama wana adhabu ya moto”*. Na mali ya uma ni ina haki zaidi ya kulindwa.

Utaifa wa kweli unapelekea pia kuunga mkono vinavyozalishwa nchini ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa viwandani kilimo biashara na masomo vinavyopelekea kukuza uzalendo wa nchi na kufikia ustawi wa kiuchumi kwa wananchi wake, kila tunapofanya juhudi kwa kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa ndio tunapo ongeza uwezo wa nchi yetu kiuchumi, na kila tunapopokea bidhaa za nchi kuuza kununua na kufanya biashara ndio tunapowapa wazalishaji na watengenezaji wa bidhaa fursa ya kuinuia uwezo wa ushindani, na kuchangia katika kuimarisha fursa zaidi za kazi kwa watoto wetu.

Kama vile kunapelekea kuheshimu mfumo wa utawala wa nchi na kulazimika kufuata sheria ambapo ni lazima kwa kila kundi katika jamii kuiishi baadhi ya mifumo na sheria ambazo zinasimamia tabia za watu na kulinda haki za mwanadamu na kulazimisha kutekeleza yaliyowajibu, tafauti na kuwepo kwa mfumo basi watu hawatapata haki zao wala kufikiwa uadilifu, kwani kuwajibika na sheria ni katika mwenendo wa kidini na kiustarabu, kusaidia nchi ni jambo la lazima ili kulinda nchi usalama wake utulivu wake na maendeleo yake.

Hotuba ya Pili.

Shukrani ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, swala na salamu zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na Watu wake na Maswahaba zake wote.

Kwa hakika uzalendo wa kweli unapelekea kushiriki kwa nia safi katika kujenga nchi, na hilo linakuwa kupitia ufanyaji kazi wa kweli na ubora wa uzalishaji bidhaa mbali mbali zikazopelekea maendeleo na ustawi kwa nchi, kwani dini yetu ya msimamo wa kati na kati haihitaji kwa watu kufanya kazi tu bali inahitaji kufanya kwazi kwa ufanisi mkubwa na uzuri ambapo anasema Mtume wetu Muhammad S.A.W *“Hakika Mwenyezi Mungu anapenda mmoja wenu anapofanya kazi basi afanya kwa umakini zaidi”*.

Na wamesema: Pindi unapotaka kujua utendaji wa mtu basi angalia ni namna gani utiifu na ufuasi wake kwa nchi yake na uzalendo wake kwa nchi yake na ufanisi wake kazi kwa ajili ya nchi yake.

Hivyo tunahitaji sana kuimarisha juhudi za jamii nchi katika kujenga nchi, kwani nchi ya wananchi wote, na yenyewe ipo kwa ajili yao na kwa juhudi zao na jasho lao wote kila mmoja katika eneo lake na uwanja wake, mwanajeshi na polisi ni jukumu lao kulinda amani ya nchi na usalama wake, daktari jukumu lake lipo kweneye hospitali yake, mkulima kwenye shamba lake, mfanya kazi katika kiwanda chake, mwanafunzi jitihada zake katika kupata elimu, na mfano wa hivyo katika uzalishaji mwingine na katika kazi zengine za mikono na wajibu mbalimbali, ambapo Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **{Saidianeni kwenye wema na ucha-Mungu na wala musisaidiane kwenye dhambi na uadui}**.

Mwenyezi Mungu tunakuomba uhifadhi Misri yetu na nchi zengine za Kiarabu na Kiislamu.